The University of Osaka
Institutional Knowledge Archive

| | |
|---|---|
| Title | Usawiri wa Shujaa wa Kike katika Utenzi wa Howani Mwana Howani |
| Author(s) | Mzee, Aboud, Fatma; Ali, Iddi, Saumu; Juma, Pembe, Riziki |
| Citation | スワヒリ＆アフリカ研究. 2014, 25, p. 162-170 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/72987 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Usawiri wa Shujaa wa Kike katika Utenzi wa Howani Mwana Howani

Fatma Aboud MZEE, Saumu Iddi ALI, Riziki Pembe JUMA

Makala haya kwanza yanaeleza utangulizi ambao utakuwa na utangulizi, usuli wa mtunzi wa kitabu na usuli wa kitabu. Katika sehemu ya pili ni kiini cha makala ambacho kitafafanua hoja ya makala haya ambayo yana usawiri wa shujaa wa kike katika utenzi wa Howani Mwana Howani na sehemu ya tatu ni hitimisho ambayo ni majumuisho na mawazo ya wawasilishaji.

## 0. Utangulizi

Kila jamii duniani ina utamaduni wake, na hivyo ndivyo ilivyo kwa jamii ya Wazanzibari. Utamaduni ni jumla kuu inayokusanya mambo yote ya asili yanayotendeka katika jamii hiyo. Hayo ni kama vile lugha, mila, itikadi, desturi, harusi, maziko, ngoma, dini, malezi, mavazi, na hata tabia. Mazingira na historia pia huchangia sana mwelekeo wa utamaduni na kuusababisha uwe hivyo ulivyo.

Mojawapo ya njia kuu za kudumisha utamaduni wa Wazanzibari baada ya ile ya vitendo vya kila siku kama vile lugha, harusi, na vinginevyo ni masimulizi ya wazee kwa watoto na wajukuu wao. Masimulizi hayo yaliwajengea watoto hisia za kupenda na kuthamini mambo mema na kuchukia mambo maovu.

Kwa bahati mbaya ulimwengu tunamoishi sasa umegubikwa na wingu la mabadiliko, mabadiliko ya ghafla yenye sura ya mapinduzi. Hapana shaka tunaishi katika zama za mapinduzi ya fikra, mila nyingi za kale, mengi ya yale tuliyokuwa tukiyathamini, sasa yanaonekana ni upuuzi mtupu au upotevu wa wakati. Uvumbuzi wa redio, televisheni, simu za mezani na za mkononi, mtandao na utandawazi kwa jumla umepindua mambo mengi katika utamaduni wetu. Ndio maana mtunzi wa kitabu hiki Bi. Zaynab hapana shaka analiokoa jahazi lililobeba shehena ya utamaduni wa Wazanzibari ili lisizame na kupotea kabisa kabisa kwa vizazi vijavyo kwa kuyahifadhi katika tungo zake.
(Nukuu ya dibaji ya kitabu iliyotolewa na Rais mstaafu wa Tanzania Mzee Ali Hassan Mwinyi.)

## 1. Usuli wa Mtunzi

Bi. Zaynab Himid alizaliwa tarehe 12 Febuari 1918 katika mtaa wa Malindi, Unguja. Alianza shule tarehe 1 Juni 1927 huko Forodhani, Unguja akiwa ni miongoni mwa wasichana wachache wa Kiafrika walioanza kusoma shule huko Zanzibar. Hii ilitokea baada ya wazee wake kumbadilisha jina kwenye cheti chake cha kuzaliwa ili aonekane kama Mwarabu ili apate nafasi shuleni. Alisoma kwa

shida kwani walipokuwa wakienda shule walirushiwa mawe njiani kwani mtazamo wa jamii wa wakati ule ulikuwa ukiona kuwa mtoto wa kike hatanufaika na elimu ya magharibi.

Mwaka 1934, Bi. Zaynab alifaulu na kuwa miongoni mwa walimu wanafunzi ambao akisoma masomo ya darasa la saba na nane kwa baadhi ya masaa na huku akisoma mafunzo ya ualimu .

Mwaka 1936 alianza kazi ya ualimu katika shule ya Town Primary mjini Unguja. Na mwaka huo huo Bi. Zaynab aliolewa na mtoto wa shangazi yake akiwa na miaka kumi na nane. Mwaka 1938 Bi. Zaynab alipata uhamisho wa kwenda kusomesha Pemba na alikuwa mwalimu mkuu wa shule ya Chachani na baada ya hapo alisomesha shule mbalimbali za Zanzibar. Aliwahi kutunukiwa nishani ya daraja la pili ya Brilliant Star na Mfalme Abdalla bin Khalifa mwaka 1963.

Alipata uzoefu wa kuandika alipokuwa shule akiandika ripoti, hotuba, michezo ya kuigiza kwa ajili ya kuigizwa na watoto wa shule na aliwahi kutunga mashairi mbalimbali ambayo yalisomwa kwenye sherehe mbalimbali. Kazi alizowahi kutunga ni kama vile shairi linalohusu Muungano, shairi la kumsifu Mwalimu Nyerere lililoitwa *Nyerere Raisi Mwema Mwenye Busara na Hima*, na pia alitunga na kuandika mchezo wa kuigiza uitwao *Unguja ya Leo si ya Jana* akishirikiana na kikundi cha Culture na pia alitunga shairi lililosomwa katika sherehe za miaka mitano tokea Nyerere awe raisi.

Bi. Zaynab aliolewa vyuo vitatu lakini hakubahatika kupata mtoto na alifariki mwaka 2002 kabla kitabu chake hakijachapishwa.

## 2. Usuli wa Kitabu

Kitabu cha *Howani mwana Howani* ni kitabu kilichokusanya tenzi mbili. Nazo ni “Howani mwana Howani” ambao umeanzia ukurasa wa 1 hadi 29 na una jumla ya beti 398 na utenzi wa pili ni “Utenzi wa Mwanakukuwa” ulioanzia ukurasa wa 40 hadi 127 na una jumla ya beti 1228.

## 3. Utenzi wa Howani Mwana Howani

Ni utenzi unaoelezea wasia autoao mama kumpa binti yake kwa kurejelea ubeti wa 1 mwandishi anasema:

> Huu wasia ushike
> Zingatie uamke
> Wewe mtoto wa kike
> Haya ziweko usoni

Utenzi unaendelea kwa kuonyesha mama tokea alivyobeba ujauzito na shida alizozipata za ujauzito huo. Kwa kurejelea ubeti wa 7:

Mimba niliichukuwa
Tumboni mwangu ukawa
Na hakika sikujua
Kilikuwa  kitu gani

Utenzi unaendelea kwa kuelezea namna mtoto mchanga anavyolelewa kwa malezi ya Kizanzibari na mambo muhimu afanyiwayo mtoto na mama mzazi tokea siku ya kujifungua hadi siku ya arobaini na kuendelea. Mambo kwa mfano mtoto mchanga kupakwa wanja ili sura yake isionekane kwa kuhofia mahasidi na wadudu wabaya, kufungwa mivuje, kuwekewa kaa, ndimu, kiwembe katika mto wa kulalia kama inavyoonekana katika beti za 68, 69, 138,139:

Wakati anapolala
Ile ile yake mila
Kutonwa kila mahala
Awazibe mashetani

Mambo anayofanyiwa mama mzazi kama kulalia moto, kukaa ndani siku arobaini haya yanaonekana katika beti za 76, 77, 78, 79, 88, 89.   Siku ya arobaini mtoto hupewa jina, na husomewa dua.

Mimi nahesabu siku
Mchana hadi usiku
Nimekaa dukuduku
Na nje nakutamani

Utenzi unaonyesha makuzi ya mtoto Mwanakukuwa anapelekwa chuoni (madrasa) ubeti wa 159 na baada ya kuhitimu chuoni hukaa nyumbani akifundishwa kazi za jikoni kama vile ubeti wa 192 unavyoeleza, na pia mtoto hufundishwa dini na kazi za amali kama vile kushona na kupakasa ukili.

Akivunja ungo  hupekekwa kwa somo ubeti wa 237  huko hufundwa mambo kwa ujumla kama vile usafi, urembo na tabia nzuri kwa ujumla tukirejelea ubeti wa 237. Utenzi unamalizia kwa kuonyesha mama mzazi anavyompa binti yake mawaidha ya dini na dunia kama vile asiwe fatani, mwizi, asiwe mzinifu, mlevi na akae na jamaa zake  kwa wema  kama katika beti za 337, 343, 360, 375 na anamalizia kwa kuhimiza na kuonyesha wanajamii kuwa ulezi ni kazi.

## 4. Utenzi wa Mwanakukuwa

Utenzi huu ni mwendelezo wa ule utenzi wa mwanzo mwandishi anathibitisha kwa kusema katika ubeti wa 3:

Azima kuendeleza
Ule utenzi wa kwanza
Mimba nalipochukuza
Nikamzaa mwandani

Utenzi unaelezea ada za mwari anapokuwa kwa somo yake kwa mfano beti za 11 mpaka 21:

Siku saba zikaisha
Somo akamfundisha
Mzuri kamrudisha
Akarudi nyumbani

Mtoto anaporudi nyumbani mzazi huwa na wasiwasi mpaka mtoto atakapoolewa kwa kurejelea ubeti wa 28, Bi. Zaynab anaendelea kutujuvya ada za mwanamwari wa Kizanzibari huwa hatoki ndani ubeti wa 32. Utenzi pia unaelezea ada za watu wa Zanzibar za kuwatafutia watoto wao wa kiume wachumba, hutumwa mtu akapeleleze tabia za mchumba mtarajiwa kama inavyoonyeshwa katika beti za 62 mpaka 79, kwa mfano watu huenda kwa mtindo wa kuuliza hali, au labda kuomba chumvi ili amkute mwanamwari katika hali yake ya uhalisia.

Mwandishi anaonyesha wajibu wa mke kumfanyia mume kama vile kumpokea mizigo anaporudi kazini, kumwandalia chakula mfano katika beti za 91, 95, 96, 97, 98, 99, 100 na 106.

Bi. Zaynab pia analieleza suala la posa, vipi posa hutolewa, mahari na sherehe nzima ya harusi kwa ujumla. Kwa mfano hutumwa mshenga kwenda kuposa na hupewa muda ili wachunguzane tabia upande wa wanaume na upande wa wanawake baadaye ndio hutolewa jawabu la kukubaliwa au kukataliwa. Ndipo mahari hutolewa na hupangwa siku ya harusi.

Utenzi pia unaelezea mambo yanayofanyika kabla ya harusi kama watu kwenda kwa mashehe kutazamia siku na wakati wa kufunga ndoa hukutana na kupanga siku ya ndoa. Maandalizi ya harusi nayo pia yameelezwa kwa kina, kuna kutazamia wakati mwafaka kwa bwana harusi kuingia kwa mkewe, mambo haya hufanywa kwa mashehe na pia wazee hukutana na kupanga namna wanavyotaka kuifanya harusi yao kama kupanga karamu na sherehe gani wafanye kama ni maulidi au taarabu.

Utenzi unamalizia kwa kuonyesha mambo yanayofanywa baada ya harusi kama swali zima la fungate ya siku saba. Katika kipindi hiki maharusi hupewa mafunzo ya namna ya kuishi kama mke na

mume na majukumu na wajibu wa mke na mume na fungate ikimalizika huenda kuhamia nyumbani kwao na kuanza maisha mapya. Mwandishi pia amelizungumzia swala la mwanamke kukutwa bikira na thamani yake kwanza wazee huonekana wamefanikiwa katika malezi na pia mwanamke hutunzwa na wakwe zake zawadi za thamani.

## 5. Shujaa wa Kike kama Anavyojitokeza katika Kitabu cha *Howani Mwana Howani*

Katika utenzi huu kunajitokeza mashujaa wa kike tofauti na tendi nyingi ambazo humchora mwanamume kuwa ni shujaa. Mashujaa waliojitokeza humu ni Mwanakukuwa na mama yake Mwanakukuwa.

Kwa kutumia ruwaza ya shujaa ya Joseph Campbell ambayo ina hatua tatu. Nazo ni kujitenga, kufundwa na kurejea.

**<Kujitenga>**

Katika hatua hii shujaa hujitenga na jamii yake yaani huondoka kwa muda. Katika Utenzi Mwanakukuwa, Mwanakukuwa baada ya kuvunja ungo anaonyesha kuwa alipelekwa kwa somo yake, hivyo alitengwa na familia yake kama mwandishi anavyosema katika ubeti wa 237.

Uwarini kapelekwa
Kwa somoye heka heka
Ili asije kuchekwa
Na wenziwe hadharani

**<Kufundwa>**

Hii ni hatua ya pili, katika hatua hii Mwanakukuwa anapewa mafunzo baada ya kuvunja ungo na pia baada ya kuposwa kwa ajili ya harusi. Mafunzo kama usafi, utanashati, dini, mila, na desturi haya yote Mwanakukuwa anafundwa na somo yake na pia na mama yake wakati wote wanapokuwa pamoja. Mafunzo haya yanaaminiwa kuwa humjenga mwanamke kuwa mke bora na atakayeitunza vizuri familia yake. Kwa mfano katika ubeti wa 241 Bi. Zaynab anasema:

Kumfundisha tohara
Asije akacharara
Kumfundisha na majira
Na mengine mema maoni

Pia katika beti za 271, na 21 zinazungumzia mafunzo aliyokuwa akipewa Mwanakukuwa.

**<Kurejea>**

Hii ni hatua ya mwisho ambapo shujaa hurejea na hupata ushindi. Baada ya kufundwa Mwanakukuwa anarudi nyumbani na kuwa mtoto mzuri na anapoolewa harusi yake inajibu baada ya kukutwa bikira. Kitendo hiki ndicho huleta ushindi na ukombozi kwa wazazi wake, upande wa mume wake na jamii kwa ujumla. Bi. Zaynab anayaonyesha haya katika beti za 648 na 647 mama yake Mwanakukuwa anasema:

Uso umenifunua
Bila tabu Bi Kukuwa
Na bwana kaulimbuwa
Hongerani hongerani

Katika mila za Kizanzibari mtoto wa kike anapoolewa kama hakukutwa bikira huwa anawaaibisha wazee wake na wazee huonekana kuwa ulezi umewashinda na kwa muktadha huu ushujaa unakosekana. Ushahidi wa haya Bi. Zaynab anasema katika ubeti wa 595:

Akambwa mtoto wao
Bikira hakuwa nayo
Aibu kubwa iliyo
Kitokea mathalani

Vile vile kama bibi harusi hakukutwa bikira huwa anapunguza mapenzi kutoka kwa wakwe zake na pia mumuwe huwa hamwamini kwa kiwango kikubwa. Harusi nayo ikijibu bibi harusi hutunzwa zawadi za thamani na mara nyingi ni mapambo ya thamani kama vile dhahabu, kiwanja cha kujengea nyumba au zawadi yoyote iwayo.

Mwanakukuwa naye katika kuonyesha ushujaa wake ni kwa kuweza kujitunza utu wake mpaka siku yake ya kuolewa na pia kustahamili mikiki na vishindo vya kuingiliwa na kutolewa bikira siku ya harusi yake. Hivyo mwandishi anatuonyesha ushujaa si kupigana vita tu bali kwa mwanamke ni kujitunza utu wake hadi siku ya kuolewa na kustahamili vishindo vya kuingiliwa na kutolewa bikira, mambo haya kwa mwanamke ni ushujaa wa hali ya juu kama walivyo kina Sundiata, Kanyamaishwa na mashujaa wengineo.

Shujaa wa pili ni mama yake Mwanakukuwa ambaye anaoneshwa ana sifa ya ushakii na anapata ujauzito ambao unamtesa sana lakini anavumilia na pia siku ya kujifungua alistahamili machungu ya uchungu hadi akajifungua salama. Huu ni ushujaa mkubwa sana kwani wako wanawake

walio wengi kutokana na sababu mbalimbali wanashindwa kufikia ushujaa wa kubeba mimba ambayo ilimtesa mpaka kujifungua kwake, na pia anastahamili machungu ya wakati wa kujifungua na pia anajitwika mzigo wa ulezi hadi mtoto anaolewa.

## 6. Utenzi wa Howani Mwana Howani nao ni Utendi?

Utenzi huu tunaweza kuuita utendi kwa sababu unafuata **kaida za muundo wa tendi** kama ifuatavyo:

(1) Kaida ya kwanza ya utendi ni **ufunguzi.** Katika kipengele hiki huwa kuna beti zinazozungumzia lengo la utendi yaani utendi utazungumzia mada gani au kisa gani, na hili linajitokeza katika tenzi zote mbili.

Katika utenzi wa mwanzo mwandishi anaelezea kuwa lengo la utenzi huo ni kumpa wasia binti yake kama anavyonukuliwa katika beti ya 5:

Huu wasia ushike
Zingatie uamke
Wewe mtoto wa kike
Haya ziweko usoni

Na pia katika utenzi wa pili mwandishi anaelezea kuwa lengo la kutunga kwake ni kuuendeleza utenzi wake wa kwanza kama katika ubeti wa 3 unavyojionyesha:

Azma kuuendeleza
Ule utenzi wa kwanza
Mimba nalipochukuza
Nikamzaa mwandani

(2) Kaida ya pili ya utendi ni **himdi.** Katika hatua hii mwandishi hutoa mwito kwa mizimu, miungu au mungu mkuu. Mtunzi huomba Mungu ampe kariha ya kumuwezesha kuusimulia au kuutongoa utendi wake, na hii imejitokeza katika utenzi huu katika beti ya 1 na 2 kwa mfano:

Bismillahi ghafuru
Nijaalie sururu
Nifunguliye na nuru
Furaha nyingi moyoni

(3) Kaida ya tatu ni **kianzio** ambapo huonyesha hatua mbalimbali za mtunzi alivyouanza utenzi wake kwa mfano huweza kuanza hadithi tokea mwanzo au akaanza katikati katika kumwelezea mhusika wake na matukio yake. Bi. Zaynab ametumia mtindo wa kiwasifu yaani matukio ya mhusika yameanza tokea kuzaliwa, kukuwa, kuoa au kuolewa. Utenzi huu wa *Howani Mwana Howani* umeanza kwa kuelezea tangu ujauzito wa mtoto Mwanakukuwa ulipochukuliwa kama inavyoonyeshwa katika ubeti wa 7:

Mimba niliichukuwa
Tumboni mwangu ukawa
Na hakika sikujuwa
Kilikuwa kitu gani.

Utenzi pia umetumia mtindo wa **in medias res** hii ni hatua ambayo nguli huoneshwa yupo katika mkondo wa masaibu yaani huanza kuonesha matukio katikati. Katika utenzi huu mama yake Mwanakukuwa anaonyeshwa yumo katika masaibu ambayo ameyapata baada ya kubeba ujauzito ambao unamtesa sana kwa kuumwa. Kwa mfano beti za 12, 14, 24, 25, na 26:

Madawa haya na yale
Yakijaa ungo tele
Wazee wapiga kile
Mwanetu yu taabani (ub wa 13)

(4) Kaida ya nne ni **mtiririko**. Katika kaida hii mtunzi huonyesha vitu mbalimbali vinavyohusika na matukio katika utendi kama vile vifaa vya vita, mashujaa na makamanda na sifa zao na nasaba zao hutajwa. Katika kufanya hivyo mwimbaji au mtunzi huwa anatoa heshima kwa wahenga na wasikilizaji wake hii ni kama ikiwa ni utenzi ni wa kivita, na kihistoria. Katika utenzi huu wa *Howani Mwana Howani* kwa vile utenzi huu unazungumzia malezi, desturi na kaida za ndoa mwandishi ameonyesha sifa za mke bora na mambo yanayotakiwa kufanyiwa mume ili ndoa idumu na kufikia hadi kupata watoto kwa mfano ubeti wa 88 mpaka 99.

Vile vile matayarisho anayofanyiwa mtoto wa kike tokea kuzaliwa kwake ili apate akue na afikie kuwa msichana. Mambo kama vile kunyonyeshwa mtoto, kupata huduma za kinga, kupelekwa madrasa, kufundishwa mila, dini, kazi za amali na kufundwa anapokuwa mwari. (rejea beti za 68, 69, 138 na 139). Pia mambo afanyiwayo bibi harusi mtarajiwa kama vile kusingwa, kupakwa hina, kupambwa na kufundishwa namna bora ya kuishi na mumewe.

(5) Kaida ya tano ni **visifa**. Katika kipengele hiki huwa kunajitokeza matumizi makubwa ya visifa vinavyoambatana na majina. Visifa katika utenzi huu wa *Howani Mwana Howani* ni jina la Mwanakukuwa lina maana ya mzazi anamwomba Mungu amkuze mtoto wake na awe mtoto mwema.

## 7. Hitimisho

Kwa ujumla Bi. Zaynab Himid anaonyesha namna mtoto wa kike anavyolelewa, kaida na mila zinazotumiwa na Wazanzibari hadi kuhakikisha kuwa malezi yamefanikiwa, katika kutimiza azma hiyo ameyahifadhi mambo haya ili yaweze kudumu kwani yamekuwa yakitoweka kila siku zinavyosonga mbele kutokana na sababu mbalimbali hasa ikiwemo utandawazi.

*Howani Mwana Howani* nao ni utendi kama zilivyo tendi nyingine ambazo huzungumzia sifa za mashujaa wa kivita lakini utenzi huu badala ya kumwelezea shujaa mwanamume, humu amesawiriwa shujaa wa kike katika mazingira ya kifamilia, ameonyeshwa kutumia ushujaa wake katika kuijenga jamii katika maadili bora. Hivyo ni kuudhihirishia umma wa wasomaji kuwa shujaa wa kike yupo na hujitokeza katika tendi nyingi za Kiswahili kama vile wanavyosawiriwa mashujaa wa kiume. Mifano ya tendi zenye mashujaa wa kike ni *Utenzi wa Rukiza* na *Utenzi wa Rasil Ghuli*.

## Marejeleo

Mohammed, Z. H. 2004. *Howani Mwana Howani*. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. 2012. *Kitini cha Utendi wa Kiswahili* .(Hakijachapishwa). Kitini kimeandikwa kwa ajili ya mihadhara ya wanafunzi wa M.A, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.